Zimeteremshwa kwangu aya, hazijawahi kuonekana mfano wake katu, sura mbili za kinga

Imepokelewa kutoka kwa Uqba bin Aamir -radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- amesema: Amesema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: "Zimeteremshwa kwangu aya, hazijawahi kuonekana mfano wake katu, sura mbili za kinga"

[Sahihi] [Imepokelewa Imamu Muslim]

Ameeleza Ukba bin Aamiri radhi za Allah ziwe juu yake yakwamba Mtume rehema na amani ziwe juu yake alisema kumwambia: Usiku huu Mwenyezi Mungu kaniteremshia aya, hazijawahi kuonekana mfano wake katu -yaani katika kuomba kinga- nazo ni sura mbili za kinga: Suratu (Qul Auudhubirabbil falaq), na suratu (Qul Auudhubirabbin naas).

http://sunnah.global/hadeeth/sw/show/65448